JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA KILIMO**

**BODI YA KOROSHO TANZANIA**


Simu: (023) 2333303
Nukushi: (023) 2333536
Baruapepe: info@cashew.go.tz
Tovuti: www.cashew@go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu,
Bodi ya Korosho Tanzania,
74 Barabara ya TANU,
S. L. P 533,
**63104 MTWARA**


**Unapojibu tafadhali taja:**
**Kumb Na.AC.118/318/01A/7**

25 Novemba, 2025

# TANGAZO LA AJIRA YA MUDA

**Nafasi:** Receptionist (Mhudumu wa Mapokezi) II – 1

**Aina ya Mkataba:** Mkataba wa mwaka mmoja (1 Year Contract)

**Mahali pa kazi:** Bodi ya Korosho Tanzania – Makao Makuu

**Maelezo ya Kazi:**

Bodi ya Korosho Tanzania inatangaza nafasi ya kazi kwa mtu mwenye uwezo, nidhamu, na uelewa wa kazi za mapokezi. Mtu atakayechaguliwa atakuwa na jukumu la kupokea wageni, kujibu simu, kutoa taarifa sahihi kwa wateja, na kuhakikisha huduma bora katika eneo la mapokezi.

**Majukumu Makuu:**

- Kupokea na kuwakaribisha wageni wanaoingia ofisini.
- Kujibu simu na kuelekeza simu kwa wahusika husika.
- Kuhifadhi na kupanga miadi ya wateja.
- Kutunza taarifa muhimu za wageni na wateja.
- Kuhakikisha eneo la mapokezi linakuwa safi na lenye mpangilio.
- Kusaidia katika kazi ndogondogo za kiutawala inapohitajika.

**Sifa za Mwombaji:**

- Awe na elimu ya angalau **Kidato cha Nne (Form IV)** au zaidi;
- Uzoefu wa kazi ya mapokezi au huduma kwa wateja utapewa kipaumbele;
- Uwe na **stadi nzuri za mawasiliano** (kwa Kiswahili na Kiingereza);
- Uwe na **muonekano wa kitaalamu na nidhamu kazini**;
- Uwe na **ufahamu wa matumizi ya kompyuta** (Microsoft Office, barua pepe, n.k.).

**Muda wa Mkataba:**

Mkataba wa mwaka mmoja (1) wenye uwezekano wa kuongezwa kulingana na utendaji kazi.

**Jinsi ya Kuomba:**

Tuma barua ya maombi ikifuatana na wasifu binafsi (CV) na nakala za vyeti husika kupitia:

Mkurugenzi Mkuu,
Bodi ya Korosho Tanzania,
Sanduku la Posta 533,
**MTWARA.**

**Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 08/12/2025 saa 10 : 00 jioni.**

Mohamed R. Muhidini
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**



Mkurugenzi Mkuu, Bodi ya Korosho Tanzania, S.L.P 533,74 Barabara ya Tanu,63104 Mtwara Simu (023)233303,Nukushi: (023)2333536 Baruapepe:info@cashew.go.tz, Tovuti;www.cashew@go.tz